



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**KUSOGEZWA MBELE KWA TAREHE YA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU
LA WAPIGA KURA
KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA YA “BIOMETRIC VOTERS REGISTRATION”
(BVR)
MKOA WA DAR ES SALAAM**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepokea maombi kutoka kwa Wadau wa Uchaguzi wakiomba kusogeza mbele tarehe ya kuanza kwa Zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ambalo lilikuwa lianze tarehe 16/07/2015.

Wadau hao wa Uchaguzi wanaomba Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa Mkoa wa Dar es Salaam usogezwe mbele ili kutoa fursa kwa wananchi kusherehekea sikukuu ya Eid-El-Fitr ambayo inatarajiwa kufanyika katika tarehe ambazo Zoezi la Uboreshaji lingeanza.

Tume imezingatia kwa uzito maombi hayo na kuamua kusogeza mbele tarehe ya kuanza kwa Zoezi la Uandikishaji wa Wapiga Kura kwa Mkoa wa Dar es Salaam. Hivyo, Zoezi hilo sasa litaanza tarehe **22/07/2015** na kumalizika tarehe **31/07/2015**

Tume inatoa wito kwa wananchi wote wa Mkoa wa Dar es Salaam kujitokeza kwa wingi katika Vituo vya Kuandikisha Wapiga Kura vilivyopo karibu na maeneo yao na kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Uandikishaji huu unawahusisha pia wananchi wa Kata ya Bunju na Mbweni ambao waliandikishwa wakati wa Zoezi la Majaribio.

Imetolewa na

Jaji Mstaafu Damian Z. Lubuva
MWENYEKITI
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI